Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ni nini ?

Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ni kampeni ya kimataifa iliyoanzia kwenye mkutano wa kwanza wa Taasisi ya Uongozi wa Wanawake Duniani (Women's Global Leadership Institute) uliofadhiliwa na Kituo Cha Uongozi wa Wanawake Duniani (Center for Women's Global Leadership) mwaka 1991. (. Washiriki walichagua tarehe 25 mwezi Novemba, Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukatili Dhidi ya Wanawake, na Desemba 10, Siku ya Haki za Binadamu Duniani, ili kuhusianisha ukatili dhidi ya wanawake na haki za binadamu na kuhamasisha kuwa ukatili kama huu ni ukiukaji wa haki za binadamu. Kipindi hiki cha siku 16 pia kinaangalia siku nyingine muhimu, ikiwemo tarehe 29 Novemba, ambayo ni Siku ya Watetezi wa Haki za Binadamu, Desemba 1 Siku ya Ukimwi Duniani na Desemba 6, Kumbukumbu ya Mauaji ya Montreal

Siku 16 za kupinga Ukatili wa Kijinsia zimekuwa zikuhudhuriwa na watu binafsi pamoja na makundi duniani kote wanaotumia mtizamo wa haki za binadamu ili kutoa mwito wa kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake kwa:

- Kuelimisha kuanzia ngazi ya jamii, kitaifa, kikanda na kimatiafa
- Kuimarisha harakati
- Kuunganisha harakati za ndani na kidunia
- Kutoa fursa ya majadiliano na kushirikishana mikakati
- Kulazimisha serikali kutekeleza maazimio ya kisheria yaliyofikiwa kitaifa na kimataifa
- Kuonyesha ushirikiano wa wanaharakati duniani

Ukatili dhidi ya wanawake ni nini?

"Ukatili dhidi ya wanawake pengine ni kitendo cha aibu cha ukiukwaji wa haki za binadamu. Na pengine ni kitendo kilichoenea Ukatili hauna mipaka ya kijiografia, mila na hata malil Kadri tunavyoendelea, hatuwezi kudai kuwa tunapiga hatua nzuri kuelekea usawa, maendeleo na amani."

Kofi Annan, Katibu Mkuu wa zamani wa Umoja wa Mataifa
"Dunia isiyokuwa na Ukatili Dhidi ya Wanawake"
Umoja wa Mtaifa Mkutano wa Dunia kwa Njia ya Video, 8 Machi 1999

Ukatili Dhidi ya Wanawake ni ukiukwaji ulionea wa haki za bianadamu , ni janga la kiafya katika jamii, na kikwazo cha kufikia usawa, maendeleo, usalama na amani. Maneno "ukatili dhidi ya wanawake" na "ukatili wa kijinsia" yanatumika kumaanisha mlolongo wa unyanyasaji unaofanyika dhidi ya wanwake unaotokana na kukuwepo na usawa wa kijinsia na hadhi ya chini wa wanawake katika jamii ukilinganisha na wanaume. Mwaka 1993, Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake uliutafasiri ukatili dhidi ya wanawake kama" kitendo chochote cha ukatili wa kijinsia kinachosababisha au kinchoweza kusababisha maumivu au mateso ya kimwili, kingono au kiakili kwa wanawake, ikiwamo vitisho, kulazimishwa au kunyimwa uhuru, vinavyotokea katika jamii au kwenye maisha binafsi ." Tafasiri hii inahusisha ukatili unaotokea kwenye ngazi ya familia, ndani ya jamii na pia ukatili unaosababishwa au kufanywa na Serikali.Aina za ukatili wa kijinsia ni pamoja na : ukatili wa majumbani,,unyanyasaji wa kingono, ubakaji, kudhalilishwa kingono,, biashara ya kusafirisha wanawake, kulazimishwa kufanya biashara ya ngono, ana vitendo vya ukatili.Kwa kuongezea,utambulisho mbalimbali wa wanawake unaozingatia tabaka, rangi,kabila, dini,mahusiano ya kingono, hali ya utaifavinaweza kuchochea ongezeko la hali ya uwezekano wa wanawake kuwa katika hali ya hatari dhidi ya ukatili.. Inakadiriwa kuwa mmoja kati ya wanwake watatu duniani atakumbana na ina Fulani za ukatili wa kijinsia katika maisha yake[1]

Mfumo wa haki za binadamu ni nini?

"Kwa kuweka masuala yanatiliwa shaka na matazamio ya wanawake katika mfumo wa haki za binadamu, tumeweza kutoa pendekezo ambalo halitaachwa: kwamba wanawake ni binadamu, na kwamba, kulingana na hilo, wanadai na wana haki zote muhimu na uhuru uliojikita katika ubinadamuy."

Florence Butegwa

[1] Heise, L., M. Ellsberg and M. Gottemoeller. 1999. *Ending Violence Against Women*. Population Reports, Series L, No. 11. Baltimore: Johns Hopkins University School of Public Health, Population Information Program.

Kwa kutumi mtizamo wa haki za binadamu ili kupingana na ukatili dhidi ya wanawake ni kitu muhimu katika Kampeni ya Siku 16 . Wanaharakati wametumia mfumo wa haki za binadamu ili kubadilisha jinsi uelewa duniani juu ya ukatili dhidi ya wanawake. Mfumo wa haki za binadamu unatambua kuwa wanawake wana haki ya kulindwa, kutambiliwa na kutimiziwa haki zao za kibinadamu kama nusu moja ya ubinadamu Mfumo unatoa lugha muhimu na nyenzo ili "kutafasiri, kuchambua na kuelezea uzoefu wa wanawake juu ya ukatili na kutaka kushughulikia katika njia ambayo inatambuliwa kimataifa"..."[2] Unyanyasi dhidi ya wanawake hauwezi kuendelea kuchukuliwa kama nyanja "binafsi",, na uwajibikaji wa Serikali unahitajika ili kuinua maazimio yjuu ya waki za wanawake kibinadamu kama yalivyofikiwa kwenye mikataba na nyaraka za kimataifa katika mfumo wa Umoja wa Mataifa Mtizamo wa haki za binadamu unatoa mfumo maalum unaoleta wanawake wenye uzoefu tofauti pamoja ili kuungana katika mikakati ya kiubunifu ili kuleta mabadiliko.

Mfumo wa haki za binadamu umetumiwa na Asasi zisizo za Kiserikali kwenye ngazi ya jamii, kitaifa na kimataifa ili kuimarisha shughuli zao dhidi ya ukatili wa kijinsia. . Kama mkakati, mfumo wa haki za binadamu unweza kuelezewa katika kanuni saba::[3]

1. **Utu**: Nguzo kuu ya haki za binadamu ni kulinda na kuboresha utu wa binadamu.
2. **Umoja duniani**: Umoja Duniani haumaniishi kuwa unakuwa sawa kwa watu wote kwa pamoja. Umoja duniani unamaanisha selikali na jamii ziweze kutambua maadili ya kiroho na kitamaduni ambayo yako kwenye sehemu zote duniani.
3. **Usawa na kutokubaguana**: Azimio la Haki za Binadamu na nyaraka nyingine za kimataifa za haki za binadamu zinaweka hazi hizohizo na majukumu sawa kwa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana wote, kwa kuzingatia utu wao pasipokujali majukumu yao au mahusiano wanayoweza kuwa nayo. Wakati ukatili dhidi ya wanawake usipotambuliwa kama unyanyasi wa haki za binadamu, wanawake kwa pamoja wanaacha kutaminiwa kama viumbe hai na kunyimwa haki zao za kiutu..
4. **Kutogawanyika**: Haki za wanawake zinapaswa kushughulikiwa kama kitu kisichogawanyika, ikiwemo, kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na haki za kiujumla.. Hizi haziwezi kupewa "kipaumbele" au kugawanywa katika "vizazi" vya haki, baadhi ziweze kupatika kabla ya nyingine.
5. **Muingiliano**: Wasi wasi katika masuala ya haki za binadamu unatokea katika Nyanja zote za maisha-– nyumbani, shule, sehemu za kazi, uchaguzi, mahakama n.k. Ukiukaji wa haki za binadamu unamuingiliano; upotevu wa haki za binadamu kwenye eneo moja unaweza kumaanisha upotevu wa haki za binadamu sehemu nyingine.. Wakati huo huo, ukuzaji wa haki za binadamu katika eneo moja unasadia ukuzwaji wa haki hizo sehemu nyingine
6. **Wajibu wa Serikali**: Haki za binadamu mara nyingi siyo zawadi zinazoweza kutolewa kwa matakwa ya serikali. Na pia serikali hazitakiwi kuzihodhi au kutoa kwa baadhi ya watu na si kwa wengine.. Wanapofanya hivyo, ni lazima wawajibishwe
7. **Jukumu binasfi.**Serikali siyo watuhumiwa pekee wa ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya wanawakeMashirika na watu binafsi wanapaswa kuwajibishwa; mila na tamaduni zinazowakandamiza wanawake lazima zihojiwe.

Mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu na maazimio yaliyofikiwa ndani ya Umoja wa Mataifa kushughulikia ukatili dhidi ya wanawake na inayohitaji Serikali kuchukua hatua ikiwemo Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake (CEDAW, 1979), Mkataba wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake (DEVAW, 1993),Azimio la Beijing na Ulingo wa Hatua(1995), Mkataba wa Mahakama ya Uhalifu Kimataifa (Mkataba wa Rome , 1998), Azimio la Milenia (2000) na Azimio la Baraza la Usalama 1325 juu ya Wanawake, Amani na Usalama (2000), na mengineyo. Kwa taarifa zaidi juu ya nyaraka hizi na nyinginezo, tafadhali angalia *Bibliography and Resource List.*

Miaka 21 ya Siku 16

Kihistoria, Kampeni ya Siku 16 imekuwa chombo muhimu katika kutumia mfumo wa haki za binadamu ili kupata msukumo wa kimataifa kwenye tatizo la kidunia la ukatili dhidi ya wanawake. Katika miaka ya awali (1991-1992), wanaharakati wa Siku 16 walitoa tamko na ukusanyaji sahihi kutoa mwito kwa Umoja wa Mataifa kuweka masual ya haki za wanawake kibinadamu kwenye ajenda kwa ajili ya Mkutano wa Kimataifa wa Haki za Binadamu, Juni 1993 huko Vienna, Austria. Wakati wa mkutano, tamko hilo lilikusanya karibu sahihi nusu milioni katika lugha 23 kutoka nchi 124.

[2] Bunch, Charlotte. From Mertus, J., N. Flowers and M. Dutt. 1999. *Local Action, Global Change: Learning About the Human Rights of Women and Girls*. UNIFEM and the Center for Women's Global Leadership.
[3]Mertus, J., N. Flowers na M. Dutt, Mwaka 1999.

Tamko lilisaidia kupata azimio rasmi juu ya haki za wanawake kama haki za binadamu na ukatili dhidi ya wanawake kama ukiukwaji wa haki za binadamu katika Azimio la ViennaPia mwaka 1999, Siku 16 za Kampeni zilikuwa ni sehemu ya juhudi zenye mafanikio kusukuma Umoja wa Mataifa kutoa tamko kuwa tarehe 25 Novemba kuwa sIku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake. Wanaharakati ngazi ya jamii, taifa na kimataifa wameweza kuona mafanikio kupitia shughuli mbalimbali pamoja na kampeni kwenye vyombo vya habari,mikutano ya vyuo, maonyesho ya sanaa, ushawishi, majadiliano ya mezani, maigizo, mahakama za kijamii na warsha.[4]

Zaidi ya mashirika 3,700 katika nchi zipatazo 164 wameshiriki katika Kampeni ya Siku 16 tokea mwaka 1991!

Kila mwaka ,CWGL inatoa mada ya kampeni kwa kujadiliana na mawakili wa haki za wanawake duniani na kusambaza tangazo la Kampeni kila mahali. Mada hizo za kila mwaka ni kama ifuatavyo:

- **1991/1992**: **Ukatili Dhidi ya Wanawake unakiuka Haki za Binadamu**
- **1993**: Demokarasia bila Haki za Binadamu kwa Wanawake . . .sio Demokrasia
- **1994**: Uelewa, Uwajibikaji, Hatua Ukatili Dhidi ya Wanawake Unakiuka Haki za Binadamus
- **1995**: Vienna, Cairo, Copenhagen, Beijing: Kuleta Nyumbani Haki za Binadamu kwa Wanawake**1996**: Kuleta Nyumbani Haki za Binadamu kwa Wanawake Kufikia Malengo Yetu
- **1997**: Dai Haki za Binadamu kwa Wanawake Nyumbani na Duniani
- **1998**: Kujenga Utamaduni wa Kuheshimu Haki za Binadamu
- **1999**: Kutimiza Ahadi ya Uhuru Dhidi ya Ukatili
- **2000**: Kusherehekea Kumbukumbu ya Miaka Kumi ya Kampeni
- **2001**: Ubaguzi wa Rangi na Ubaguzi wa Kingono Ukatili Basi**2002**: Kujenga Utamaduni wa Kusema "Hapana" kwa Ukatili Dhidi ya Wanawake
- **2003**: Ukatili Dhidi ya Wanawake Unakiuka Haki za Binadamu: Kudumisha Kasi ya Miaka Kumi Baada ya Vienna (1993-2003)
- **2004/2005**: Kwa Afya ya Wanawake, Kwa Afya ya Dunia: UKATILI ZAIDI HAPANA
- **2006**: Sherehekea miaka 16 ya Siku 16: Inua Haki za Binadamu ↔Tokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake
- **2007**: Kudai Utekelezaji, Kuhoji Vikwazo: Tokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake!
- **2008**: Haki za Binadamu kwa Wanawake ↔ Haki za Binadamu kwa Wote: Kusherehekea Miaka 60 ya Azimio la Haki za Binadamu
- **2009**: AMUA ▪ CHUKUA HATUA ▪ DAI: Tuna WEZA Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake!
- **2010**: Miundo ya Ukatili: Elezea Muingiliano wa Utawala wa Kijeshi na Ukatili Dhidi ya Wanawake
- **2011:**

Kutoka Amani Nyumbani mpaka Kwenye Amani Duniani: Tuhoji Madaraka ya Kijeshi na Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake

Utawala wa kijeshi ni dhana inayojenga utamaduni wa woga na kusaidia matumizi ya ukatili, uchokozi au uavamizi wa kijeshi katika kumaliza migogoro na kusaidia maslahi ya kiuchumi na kisiasa. Ni saikolojia ambayo mara nyingi ina athari mbaya kwa usalama wa kweli na amani kwa wanawake na jamii kwa ujumla, na hivyo kuna haja ya kushughulikia imani za utawala wa kijeshi katika jamii zetu.. Vita,migogoro ya ndani, vurugu za kisiasa za kijamii harakati za kutetea haki vimekuwa na athari fulani na zisizowiana kwa wanawake na ukatili wanaokumbana nao.. Hata katika maeneo ambayo hayana migogoro moja kwa moja hayajaachwa na utawala wa: watuma vikosi, wanatengeneza na kuuza silaha, na kuwekeza kwenye majeshi ya nchi za serikali za kigeni kuliko kusaidia juhudi za maendeleo. Kutokana na mrejesho walioupata CWGL kutoka kwa washiriki wakati wa kampani ya mwaka 2010 kampeni ya mwaka huu inazingatia mada ndogo ndogo, zinazoelezewa kwa kina katika Kasha la vielelezo vya Chukua Hatua :

1. Kujenga daraja la haki za wanawake, haki za binadamu, na harakati za amani na kuhoji utawala wa kijeshi
2. Kuenea kwa silaha ndogo ndogo na jukumu lake katika ukatili majumbani
3. Ukatili wa Kingono wakati na baada ya migogoro
4. Ukatili wa kisiasa dhidi ya wanawake ikiwemo ukatili Kabla/Wakati/ Baada ya uchaguziUkatili wa Kingono na kijinsia unaofanywa na wakala wa serikali, hususani askari polisi au wanajeshi

Tfadhali jiunge na CWGL tunapofanyakazi pamoja kusaidia uratibu wa kidunia wa hatua za wafeministi dhidi ya ukatili unaochochewa na utawala wa kijeshi.

Translated by Festa Andrew Mwanyingili, Women's Dignity

[4]Kwa taarifa zaidi juu ya matukio kwa miaka duniani, tafadhali angalia Kalenda ya Shughuli za Kidunia kutoka mwaka 1991-2010 – kwanye mtandao.